*(Masomo maalumu kwa watumishi wa Mungu).*

Katika agano la Kale, Mungu aliwafundisha Haruni *(aliyekuwa kuhani mkuu)* pamoja na wanawe wote, jinsi ya kuwabarikia wana wa Israeli, na kupitia sala hiyo, au matamko hayo wana wa Israeli walibarikiwa kweli kweli.

Sala hiyo pia inaweza kutumika na watumishi wa Mungu leo, kulibarikia kundi la MUNGU, kwani nao pia ni makuhani kwa Mungu sawasawa na *Ufunuo 1:6*

Sala hiyo tunaisoma katika *Hesabu 6:22-27.*

> *Hesabu 6:22 "Kisha Bwana akanena na Musa, na kumwambia,*
>
> *23 Nena na Haruni na wanawe, uwaambie, HIVI NDIVYO MTAKAVYOWABARIKIA WANA WA ISRAELI; MTAWAAMBIA*
>
> *24 Bwana akubarikie, na kukulinda;*
>
> *25 Bwana akuangazie nuru za uso wake, na kukufadhili;*

Sala ya baraka (Hesabu 6:24-26).

> *26 Bwana akuinulie uso wake, na kukupa Amani*
>
> *27 Ndivyo watakavyoweka jina langu juu ya wana wa Israeli; nami nitawabarikia"*

Na baraka hizo ni lazima zitamkwe baada ya watu kufundishwa kanuni za kubarikiwa, na kupokea Amani ya kiMungu na ulinzi.

Bwana akubariki.

Washirikishe na wengine habari hizi njema kwa kushea

Ikiwa utapenda kupata msaada wa kumpokea Yesu maishani mwako bure, Basi wasiliana nasi kwa namba uzionazo chini ya makala hii.

Pia kwa kupokea mafundisho ya kila siku kwa njia ya WHATSAPP, jiunge na channel yetu kwa kupofya link hii >> https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx1

Kwa mawasiliano: +255789001312 au +255693036618

Sala ya baraka (Hesabu 6:24-26).

Bwana akubariki.

Mafundisho mengine:

SALA YA BWANA. (Namna ya kuiomba)

FIMBO YA HARUNI!

TOBA IGUSAYO MOYO WA BWANA.

Ni lazima mtu aongozwe sala ya toba ili awe ameokoka?

HARUNI

Rudi Nyumbani

Share on:
WhatsApp